



REPUBLIC OF KENYA

COUNTY ASSEMBLY OF KILIFI

SECOND ASSEMBLY –FIFTH SESSION

THE HANSARD

Wednesday, 10th March 2021

*The House met at the County Assembly Chamber,
Malindi Town, at 11:00 a.m.*

[The Deputy Speaker (Hon. Kenga) in the Chair]

PRAYERS

STATEMENTS

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Hon. Members, the Statements whose Members are not in the House will be sent back to the House Business Committee for consideration in the sittings to follow.

INEFFICIENCIES AT THE BAMBA VOCATIONAL TECHNICAL TRAINING CENTRE

Hon. Chiriba: Thank you Mr. Speaker for giving me this opportunity to rise and read a Response from a Statement sought by the able hon. Member of Bamba Ward. The Statement is about the Bamba Vocational Technical Training Centre:-

Whether the County Executive Committee Member (CECM) in charge of the Department of Education and ICT is aware that Bamba Vocational Technical Centre (VTC) has no fence and is not connected to electricity.

Whether the CECM is further aware that Bamba VTC has only one watchman who works without off-duty and has not been paid for the last six months.

If yes, what measures is the Department taking to have the VTC secured, connected to the power grid and the watchman paid?

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Mr. Speaker, in reference to the above matter I want to report to this House that the CECM is aware and that Bamba Vocational Training Centre has no fence and is not connected to electricity.

In the financial year 2019/2020 budget, the Centre had been considered for electrical connectivity but since the allocation was not sufficient to connect all VTCs that were not connected, priority was given to older VTCs that is those that that were started way back. This way, Bamba VTC was left out since it began in January 2019. The 2020/2021 budget also has not enabled the connectivity of electricity at the Centre. The VTC has in their 2021 budget of the conditional grant prioritized to initiate fencing the institution.

Bamba Vocational Training Center has got one watchman, who was initially hired by the Bamba Member of County Assembly before the VTC was operational in 2018 but eventually the VTC Board of Members officially hired him in January, 2019.

The Watchman is all alone and works at night since during the day the Centre has the instructors who take charge. However, the VTC has also not been able to engage an extra watchman as it is still young and fees payment by trainees is not good. The VTC depends on what they receive from the Ward Scholarship kitty.

Since March 2020, the VTCs like other learning institutions were closed due to COVID-19 and thus learners were sent home meaning fees payment has not been done thus resulted into salary arrears of the watchman and instructor employed by the Board.

The Department recognizes the great effort by the area Member of County Assembly and promises full support to ensure that the VTC expands and thus able to enroll more students. With the 2021 conditional grant, the Department will ensure that securing of the VTC by fencing is initiated.

The Department will in the next financial year allocate funds for electrical connectivity in the VTC; all the salary arrears of the watchman and the beauty instructor will be cleared once the VTC gets bursary for the second year students that are correctly in the VTC and have applied for bursary from the Ward Scholarship Fund. Thank you, Mr. Speaker.

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Thank you very much hon. Chairperson. Let us hear from the hon. Member who sought the Statement in the first place.

Hon. Mwambire: Asante sana Bw. Spika. Kwanza, ningetaka kusema kwamba haya majibu ambayo Waziri wa Elimu ameweza kupeana yako mwafwaka lakini yako na udanganyifu. Hii ni kwa sababu kabla niweze kupeana hii *Statement* kuna vikao ambavyo tulikaa hapo mwanzo na wakurugenzi na tukafikiana mambo fulani ili kusaidia hii shule kuweza kupeana hizi taaluma ambazo ziko hapo. Katika swala la mlinzi ambaye analinda pale pahali ni kwamba mwaka wa 2019 tuliweza kukaa kikao tukafanya mazungumzo pamoja na msimamizi wa elimu hii ya ufundi katika eneo la Ganze pamoja na msimamizi wa kile chuo.

Tulizungumza na tukaafikiana kwamba mambo haya ya madeni ya huyu mwalimu wa mambo ya urembo pamoja na mlinzi yaweze kutamatika. Na nataka kushukuru wanakamati ambao wanasimamia ugavi wa pesa ya kusaidia hali ya masomo kwa sababu waliweza kutenga pesa kwa chuo hiki ili mambo kama haya yaweza kutatuliwa. Lakini ninavyoongea hapa ni kwamba bado hali ni ile ile. Kwa hivyo, ninapoona majibu kwamba wanategemea pesa ziweze kulipwa katika sehemu ile ya kusimamia mambo ya masomo ninashangaa tutapeana pesa ngapi ili tuweze kuyafikia mambo yale ya malipo.

Bwana Spika, nikwamba Chuo cha Ufundi cha Bamba tulikiwekea shilingi elfu 200 mwanzo wa mwaka jana. Kama tulivyozungumza kwenye kikao mwaka 2019, kulikuwa na

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

walimu waliokuwa wanadai, mwalimu wa urembo aliyekuwa anadai shilingi elfu 60 na mlinzi karibia shilingi elfu 60. Matarajio yangu ilikuwa ni hizi pesa zikiingia zilipe haya madeni lakini nilipigiwa simu kwamba mwalimu wa urembo alipewa shilingi elfu 12 pekee na akaamua kuwacha kazi baada ya kwenda kushtaki katika kituo cha polisi cha Ganze. Baada ya miezi minne walikuja kudai mishahara yao na nikawaonyesha kwamba pesa nililipa kupitia kamati na hata nikawaonyesha *receipt* ya kuonyesha pesa ilifika shule. Siridhiki na majibu haya.

(Hon. Mwarandu stood on a Point of Order)

Hon. Mwarandu: Mheshimiwa Spika, Kanuni ya Bunge ya 87 kuhusu *Statements of facts*; Bunge sio mahali pa umbea na tunaongea mambo ya ukweli. Mheshimiwa aliyekuwa akiongea alikuwa anatupa historia ambayo sisi hatuwezi kuijadili, tunaomba aende moja kwa moja kwa yale mambo yaliyo hapa ama kama ana ushahidi wa mambo anayosema alete Bungeni.

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Hon. Mwambire, you have exhausted your time. Kindly go to the point as advised.

Hon. Mwambire: Kwanza napenda kumkosoa mheshimiwa Mwarandu. Mimi ndio ninasimamia Wadi ya Bamba na ninaongea kulingana na majibu niliyopewa hapa. Mheshimiwa Spika, katika maelezo ya mambo ya *fence* na kuunganishiwa umeme katika chuo kile nakubaliana nayo, lakini mambo ya malipo na kwamba watu wapewe tena *bursary* mimi bado niko na maswali na siwezi kwenda kuuliza pesa zilitumika vipi; siwezi peana *bursary* tena ikiwa ile ilipeanwa sijui inatumika namna gani. Asante na sjaridhishwa na mambo ya malipo.

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Hon. Chiriba, who is also the Chairperson?

Hon. Chiriba: Thank you Mr. Speaker. I want to thank the hon. Member who is in agreement with the larger part of the Response. The area that he has expressed doubt I can try to answer; the issue of *bursary* being mentioned here simply because as we read from the statement the employee is under the Board of Management and not an employee of the County Government. The Board will entirely depend on the fees collected and we all know that COVID-19 brought so many things to a halt and the fee collection done was not enough which can result to such concerns. If the Member can consider this, then I think somehow it can answer his questions.

Hon. Mwambire: Kama nilivyokuwa ninaeleza wakati mheshimiwa Mwarandu alipoingilia, sijakataa majibu yake lakini kuna utata katika yale mazungumzo tunayozungumza. Wakati wa kikao mambo yanaenda kinyume na vile ambavyo vinafaa. Sijakataa kupeana *bursary* pale...

(Hon. Mramba stood on a Point of Order)

Hon. Mramba: Bw. Spika, mimi kama Mwenyekiti wa ile Kamati ya *County Ward Scholarship Fund*, ninataka kumjulisha kwamba ni jukumu lake kusimamia na kuhakikisha wanafunzi wamepata *bursary*; si haki awanyime *bursary* kwa sababu hawaendi kulingana na mipangilio. Wafanyakazi walijajiriwa na chuo na mheshimiwa Daniel Mangi alikuwa anamlipa kutoka kwa pesa zake za mfukoni. Kwa hii kesi ni kwamba mheshimiwa Mwambire amewapa *bursary* na huwezi kupeana *bursary* kwa shule na uanze kuwakazia lazima ufanye hili au hilo; sio jukumu lako. Jukumu lako ni kuhakikisha wanafunzi wako wamelipiwa *fee*, matumizi ya shule yanalengana na bodi ya usimamizi wa shule. Kama kuna lolote la zaidi mheshimiwa

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Mwambire anafaa kukaa na bodi waelewane lakini jukumu la kuwapa *bursary* lazima liendeele. Hawezi kuwanyima *bursary* kwa sababu akiwapa hawalipi mshahara; hiyo sio haki.

Hon. Mwambire: Nataka kumrekebisha mheshimiwa Mramba. Hii shule nilianzisha mimi na kama ilivyoandikwa hapa kwamba mimi ndio nilikuwa ninalipa huyo mlinzi. Kuna mambo ambayo huwa tunaongea katika kikao kabla sijatuma hizi pesa kwao lakini kila wakati nikishatuma hakuna linalofanywa kusuluhisha hili tatizo la madeni.

Hon. Hassan: Asante sana mheshimiwa Spika. Jukumu la watu wa Bamba tungemuachia mwenyewe mheshimiwa wa Bamba na yeye ana hiari ya kuwa au la; maamuzi yako na hiyo bodi ya hicho chuo, cha msingi ni yeye akae na hiyo bodi wakubaliane.

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Hon. Chiriba, any submission?

Hon. Chiriba: I do not have much to submit. I pray that hon. Mwambire would understand that as the CECM has responded to the Statement satisfactorily. In case of the issues which he doubts, he can read from what the other Members are saying that the issue is for the Board and not the CECM.

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Hon. Mwambire, are you satisfied with the Response?

Hon. Mwambire: Asante Mheshimiwa Spika itabidi nikamuone Waziri *I make a special request.*

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Thank you very much. Let us settle the matter at that. If for any reasons there will be other issues, then he will be in a position to make a Statement.

KAMALA HOLDING GROUNDS

Next was on a Statement sought by hon. Kenga. This will go back to the House Business Committee for allocation of time in the next sitting.

(Statement deferred)

ADJOURNMENT

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): There being no other Business in the Order Paper, this House stands adjourned.

The House rose at 11:22 a.m.